LEGAL AND HUMAN RIGHTS CENTRE

Justice Lugakingira House, Block 44, Plot 508 & 509, Kijitonyama,
P. O. Box 75254, Dar Es Salaam, TANZANIA • Telephone: 2773048, 2773038, Fax: 2773037,
E-mail: lhrc@humanrights.or.tz Website: www.humanrights.or.tz

for a Just and Equitable Society

# HALI YA HAKI ZA BINADAMU KWA KIPINDI CHA NUSU MWAKA TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI

## JANUARI – JUNI 2015

Ndugu waandishi wa habari,

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinaendelea na utaratibu wake wa kila mwaka wa kutoa tathmini ya hali ya haki za binadamu kwa kipindi cha nusu mwaka cha miezi sita. Tathmini hii hufanywa kwa malengo ya kutoa muelekeo wa hali ya ulinzi na ukiukwaji wa haki za binadamu tunapoingia nusu ya pili ya mwaka.

Taarifa hii ni matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu, ufuatiliaji wa ukiukwaji wa haki za binadamu, pia taarifa mbalimbali kutoka kwa waangalizi wa haki za binadamu, wasaidizi wa kisheria, taarifa rasmi toka taasisi za Serikali, Bunge, Mahakama, vyombo vya habari na asasi mbalimbali za kiraia zisizo za Serikali.

Taarifa hii inajikita zaidi kuangalia maeneo machache ya haki za binadamu ambayo yameonyesha kuwa na ukiukwaji wa hali ya juu katika kipindi cha nusu mwaka. Taarifa kamili ya hali ya haki za binadamu nchini itaandaliwa mwishoni mwa mwaka.

### 1. Haki ya Kuishi

Haki ya kuishi imeendelea kuwa ni mojawapo ya haki zinazokiukwa kwa kiwango kikubwa sana. Haki ya kuishi ni haki ya msingi kabisa ambayo inatakiwa iheshimiwe kwa kila mtu. Haki ya kuishi inakiukwa kupitia mambo kama kujichukulia sheria mikononi; watu kufia mikononi mwa vyombo vya dola; mauaji na ukatili wa watu wenye ualbino; mauaji yatokanayo na imani za kishirikina; na ajali za barabarani.

**Kujichukulia sheria mikononi:**

Tafiti mbalimbali zilizofanywa na Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu zinaonyesha kuwa matukio ya kujichukulia sheria mikononi yameendelea kuwa mengi nchini. Matukio haya yamekuwa yakiwahusisha zaidi watu wanaokutwa na tuhuma za wizi, na hasa vibaka. Kwa kipindi cha nusu mwaka, taarifa kutoka Jeshi la Polisi zinaonyesha kuwa watu **366** waliuawa kutokana na watu kujichukulia sheria mikononi. Hii ni pungufu kidogo ukilinganisha na kipindi kama hiki kwa mwaka 2014 ambapo taarifa ilionyesha kutokea kwa vifo vya watu **473.** Tafiti na uzoefu unaonyesha kuwa matukio mengi yamekuwa hayatolewi taarifa kwenye vyombo vya dola, na hasa kwenye maeneo ya vijijini.

**Uvamizi wa vituo vya Polisi na Mauaji ya Askari Polisi:**



**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

Askari polisi nao pia wamekuwa wahanga wa mashambulizi mbalimbali hasa wanapokuwa kazini. Matukio ya uvamaizi yaliyokuwa yamezoeleka ni yale ya uvamizi wa vituo vya polisi yanayofanywa na watu wenye hasira kali, ambapo kwa kipindi cha nusu mwaka vituo **4** vya polisi vilivamiwa. Lakini hivi karibuni, matukio haya ya uvamizi yamehusisha makundi ya watu wenye silaha ambao wanahisiwa kuwa ni majambazi. Kwa kipindi cha nusu mwaka pekee vituo kadhaa vya polisi vilivamiwa na kusababisha vifo vya askari polisi **3**, na uporaji wa silaha mbalimbali za jeshi la polisi. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kingependa kutoa wito kwa Jeshi la Polisi na Serikali kuhakikisha kuwa vituo hivi vinakuwa na ulinzi madhubuti ili kuwawezesha askari polisi kufanya kazi katika mazingira ya amani na ulinzi wa maisha yao. Hii ni kwa sababu, ndani ya kipindi kisichozidi mwaka mmoja jumla ya askari **8** wameuawa katika uvamizi wa aina hii, na kusababisha uporaji wa silaha mbalimbali zipatazo bunduki **38** na risasi nyingi.

**Watu Kufia Mikononi mwa vyombo vya Dola:**

Vyombo vya dola vimehusishwa na kusababisha mauaji ya watu mbalimbali wakiwa chini ya ulinzi wa vyombo hivi. Taarifa rasmi ya Jeshi la Polisi inaonyesha kuwa kwa kipindi hiki cha nusu mwaka ni mtu mmoja (1) pekee ndie aliuawa akiwa mikononi mwa jeshi la polisi. Hata hivyo, Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinataarifa ya matukio ya watu **watano (5)** wanaosemekana walifia mikononi mwa vyombo vya dola, watatu wakiwa mikononi mwa polisi na wengine wawili wanaosemekana kuuawa na askari walinzi wa Pori Tengefu la Mwiba huko Meatu.

**Mauaji na Ukatili wa Watu Wenye ualbino:**

Nchi yetu imeendelea kushuhudia manyanyaso, ukatili na mauaji ya ndugu zetu wenye ualbino. Matukio haya yamekuwa yanahusishwa zaidi na imani za kishirikina ambapo kuna baadhi ya watu wamekuwa wakiamini/shwa kuwa viungo vya watu wenye ualbino vikitumika kishirikina vinaweza kumfanya mtu akapata utajiri na mafanikio katika shughuli zake mbalimbali, zikiwemo za biashara, siasa na shughuli nyingine za kujiingizia kipato. Hii imeibua hali ya kuwindwa, kushambuliwa na kuuawa kwa watu wenye ualbino ili viungo vyao vya mwili vipatikane kwa ajili hiyo. Kwa kipindi cha nusu mwaka pekee, matukio **manne (4)** yameripotiwa yanayohusisha mashambulio haya. Kati ya matukio haya, moja linahusisha kuuawa kwa mtoto wa mwaka mmoja, ambaye alitekwa kutoka kwenye mikono ya mama yake na baadae mwili wake kuokotwa porini ukiwa umekatwa mikono yote miwili na miguu yote miwili. Matukio mengine **matatu (3)** yanahusisha mashambulizi ya mwili ambapo watu wenye ualbino walikatwa mikono na miguu. Mashambulizi haya yanafanya watu walio na ualbino kuishi katika hali ya uoga wa maisha yao na hivyo kukimbia makazi yao na/au kuwapeleka watoto wao kuishi na ndugu wengine wa familia au katika makambi mbalimbali ambapo wanadhani wanaweza kuwa salama zaidi.

Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinasikitishwa sana na kujirudia kwa matukio haya hasa baada ya kuonekana kuwa yalikuwa yamepungua miaka miwili iliyopita.

**Mauaji Yatokanayo na Imani za Kishirikina:**



**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

Mauaji yanayotokana na imani za kishirikina pia yameendelea kuwa chanzo cha mauaji na mateso kwa watanzania wengi, na hasa vikongwe katika maeneo ya vijijini. Kwa kipindi cha nusu mwaka yameripotiwa mauaji ya watu **57**. Hii ni pungufu kubwa ukilinganisha na mauaji yaliyotolewa taarifa katika kipindi kama hicho kwa mwaka 2014, ambapo watu **320** waliuawa. Lakini tafiti zinaonyesha kuwa matukio mengi ya mauaji na mateso ya aina hii yamekuwa hayatolewi taarifa kwenye vyombo vya dola. Matukio mengi yamehusisha utoaji wa adhabu za kijadi kwa watuhumiwa wa watu wanaojihusisha na vitendo vya ushirikina hasa katika kanda ya ziwa ambapo wazee wa jadi walihusishwa na utoaji wa adhabu za viboko, kuchomewa nyumba na hata kufukuzwa kutoka vijiji vyao kwa watuhumiwa. Tukio kama hili lilitokea huko Serengeti ambapo watu 14 walipigwa vibaya na kufukuzwa kutoka kijiji cha Robanda, wawili kati yao walikufa baadae kutokana na majeraha waliyopata.

**Ajali za Barabarani:**

Matukio ya ajali za barabarani yameendelea kupoteza maisha ya maelfu ya watanzania na kuwaacha wengine na ulemavu wa kudumu. Tafiti zinaonyesha kuwa ajali za barabarani ni sababu ya pili kwa kusabisha vifo vingi, ikitanguliwa na ugonjwa wa malaria nchini. Kwa kipindi hiki cha nusu mwaka watu **1,548** wamepoteza maisha kutokana na ajali za barabarani. Hii inaonesha ongezeko la vifo vitokanavyo na ajali za barabarani ikilinganishwa na kipindi kama hiki kwa mwaka 2014 ambapo vifo 1,505 vilitokea. Vifo vitokanavyo na ajali za barabarani husababisha ongezeko la wajane, watoto yatima na watu walio tegemezi na kuongeza umasikini wa kipato ndani ya familia na kurudi nyuma kwa maendeleo.

## 2. Haki za Wanawake na Mtoto

Matukio ya ukiukwaji wa haki za wanawake na watoto yameendelea kuripotiwa kwa kiasi kikubwa nchini. Ukiukwaji wa haki za wanawake unafanyika kupitia ukatili wa kijinsia, ukatili wa kingono, ukeketaji na unyanyapaa wa wanawake. Matukio ya ukiukwaji wa haki za watoto yanahisisha mateso ya aina mbalimbali dhidi ya watoto, ulawiti, unajisi, kuozwa katika umri mdogo, kutumikishwa na zaidi katika mazingira hatarishi, kutupwa kwa watoto wachanga. Sheria ya Ndoa ya mwaka 1971 inaendelea kuvunja haki za mtoto kwa kutambua ndoa za utotoni kwa mtoto wa kike katika umri mdogo wa mpaka miaka 14. Tafiti mbalimbali zinaonyesha kuwa katika baadhi ya sehemu za nchi yetu, watoto 2 kati ya watoto 5 huolewa katika umri mdogo wa kati ya miaka 14 na 19. Hii ikizingatia pia kwamba ni 12% pekee ya watoto walioolewa kabla ya kutimiza miaka 19, wanatumia njia za kisasa za uzazi wa mpango. Hii inawaweka watoto hawa katika hatari kubwa ya maambukizi ya magonjwa mbalimbali lakini pia kuwa hatarini katika kipindi cha kujifungua. Ulinzi wa haki za watoto ni muhimu kwa ustawi wa jamii yetu, hasa ikizingatiwa idadi ya watoto na vijana ndio kundi kubwa zaidi kuliko kundi linguine lolote katika jamii yetu.

## 3. Haki ya Kupata Habari na Uhuru wa Vyombo vya Habari:

Nchi yetu pia imeendelea kupata changamoto katika haki ya kujieleza na uhuru wa vyombo vya habari. Mwezi Januari mwaka huu serikali kupitia Idara ya Maelezo ilitoa tamko la kufungiwa kwa gazeti la *The East African*. Sababu zilizotolewa na serikali ni kwamba gazeti hili limekuwa likisambazwa nchini bila kuwa na kibali. Jambo hili kidogo linashangaza



**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv),
Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

kwani gazeti hili limekuwa likisambazwa na kuuzwa nchini kwa takribani kipindi cha miaka 20. Serikali pia ilieleza kuwa sababu nyingine ya kufungiwa kwa gazeti hili ni mwendelezo wa gazeti hili kutoa makala ambazo zinaeneza agenda hasi dhidi ya Serikali na Nchi.

Katika kipindi hiki tumeshuhudia pia manyanyaso ya waandishi wa habari wakiwa katika kutekeleza majukumu yao. Matukio haya yamehusisha waandishi takribani watatu, likiwemo la mtangazaji wa luninga na mwandishi wa gazeti la mwananchi kupigwa na kuwekwa rumande kwa muda pale walipokuwa wakifuatilia habari zilizomuhusisha mbunge akituhumiwa kutelekeza mtoto. Lakini tukio linguine lilihusisha mwandishi wa habari wa gazeti la Mwananchi kunyimwa fursa ya kufanya kazi yake pale alipoonyesha nia ya kumuuliza swali Rais wa Ujerumani, kinyume cha maelekezo ya ofisi ya Mwandishi wa Ikulu.

Mwaka huu pia tumeshuhudia Bunge kupitisha sheria mbalimbali ambazo zinabana na/au kuvunja haki ya kupata habari lakini pia na uhuru wa kujieleza. Sheria hizi ni kama Sheria ya Takwimu na Sheria ya Makosa ya Mtandaoni. Tumeshuhudia pia serikali ikipeleka miswada ya sheria za Haki ya Kupata wa Habari na pia muswada wa sheria ya Vyombo vya Habari kwa njia ya hati ya dharura, na bila kuzingatia maoni ya wadau.

## 4. Haki ya Afya Bora

Afya bora inategemea uwepo na upatikanaji wa madawa na vifaa vya vifaa vya tiba. Utafiti ulioofanywa na shirika la SIKIKA umeonyesha kuwa hospitali za nchi zimekumbwa na upungufu mkubwa wa damu katika benki zake za damu. Upungufu huu umeelezwa kuwa unatokana na uwepo wa bajeti finyu, ambayo kwa kiasi kikubwa inafadhiliwa na Serikali ya Marekani na sehemu ndogo kufandhiliwa na serikali ya Tanzania. Kati ya wilaya zilizoonekana kuwa na upungufu mkubwa wa damu ni pamoja na Simanjiro na Mpwapwa ambazo ziligundulika kuwa na kiwango kidogo sana au kukosa kabisa akiba ya damu katika benki zao za damu kulingana na mahitaji ya mwaka ya maeneo husika. Wilaya nyingine na kiasi cha akiba ya damu iliyokuwepo ni pamoja na Temeke (20% ya mahitaji), Amana (40% ya mahitaji), pamoja na Hospitali ya Taifa ya Muhimbili (50-65% ya mahitaji ya mwaka).

Kumekuwa pia na upungufu mkubwa wa madawa katika hospitali za umma. Hii ilielezwa kutokana na malimbikizo makubwa ya madeni ya Serikali kwa Bohari ya Madawa ya Taifa na hivyo kupelekea bohari kushindwa kununua dawa kwa ajili ya kusambaza katika hospitali mbalimbali za umma nchini. Mwezi wa sita ilitolewa taarifa Bungeni kuwa deni hili limefikia Shilingi Bilioni 125.

## 5. Haki ya Kupiga Kura - Uboreshwaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura kwa Mfumo wa BVR:

Nchi yetu ya Tanzania inajiandaa na zoezi la uchaguzi mkuu ifikapo mwezi Oktoba mwaka huu. Zoezi hili linahusisha pia uboreshwaji wa daftari la kudumu la wapiga kura kwa mfumo wa kisasa wa digitali, ama Bio Metric Voters Registration (BVR). Zoezi hili linahusisha mikoa yote ya Tanzania bara, likitoa haki kwa watanzania wote walio na sifa ya kupiga kura na waliotimiza umri wa miaka 18 na kuendelea kuandikishwa ili kuweza kuandikishwa.



**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

Zoezi la uboreshwaji na uandikishaji wapiga kura kwenye daftari la kudumu lilianza tarehe 23 Machi, 2015. Zoezi hili limegubikwa na kasoro mbalimbali ambazo zinaweza kusababisha baadhi ya watanzania kunyimwa haki yao ya kikatiba kushiriki katika uchaguzi mkuu. Kasoro hizi zinahusisha vifaa vya uandikishaji, watendaji wa uandikishaji lakini pia na miundo mbinu mingine ambayo kwa namna moja ama nyingine inaathiri zoezi hili kwa namna moja au nyingine.

Miongoni mwa mapungufu hayo ni kama ifuatavyo: a) Kutokutolewa kabisa au kwa upungufu kwa elimu ya uraia juu ya kujiandikisha ambao ulipelekea watu wachache kujitokeza hasa kwa siku 2 hadi 3 za kwanza; b) Kuwepo kwa vifaa vichache vya kuandikishia wapiga kura katika maeneo mbalimbali ya nchi hasa yale yaliyokuwa na uhitaji mkubwa; c) kuharibika mara kwa mara kwa vifaa vya uandikishaji; d) Muda wa uandikishaji kuwa mchache katika maeneo mengi, siku 7 zilizotengwa hazikutosha; e) Vyama vya siasa kuingilia zoezi la uandikishaji; f) kwenye maeneo mengi watu wenye ulemavu hawakupewa huduma stahiki kulingana na mahitaji yao maalum; g) Kuwepo taarifa finyu juu ya zoezi la uandikishwaji kwenye baadhi ya maeneo na pia taarifa zisizo kamili, kama vile maeneo na muda wa kuandikishwa. Mapungufu haya yamepelekea kuwe na malalamiko ya watu wengi kukosa fursa ya kujiandikisha katika daftari la kudumu la wapigakura. Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kina taarifa ya watu kadhaa ambao wamekosa fursa ya kujiandikisha kutokana na mapungufu yaliyoainishwa.

Haki ya wananchi kushiriki kwenye uongozi wa nchi inaendelea kukiukwa nchini Tanzania. Haki hii inakiukwa kwa Katiba na sheria kuendelea kutokutambua mgombea binafsi, kinyume na maamuzi ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu ambayo iliitaka Tanzania kurekebisha Katiba na sheria zake ili kuruhusu suala hili.

Nchi yetu pia imeshindwa kufanya mabadiliko ya Kikatiba na Sheria ili kubadilisha muundo wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi ili kuwe na Tume Huru ya Uchaguzi hasa tunapoelekea kwenye uchaguzi mkuu na baada ya mchakato wa Katiba kuwa na sintofahamu.

## 6. Rushwa na Utawala Bora

Nchi yetu imekumbwa na wimbi la kashfa kubwa za rushwa zikihusisha watu muhimu katika Taifa. Mojawapo ya kashfa hizi ni ile ya akaunti ya ESCROW. Miongoni mwa watu waliohusishwa na kashfa hii ni pamoja na Majaji wa Mahakama Kuu ya Tanzania, Mawaziri, Wabunge, viongozi wa mashirika ya umma, Wajumbe wa Bodi za Mashirika ya Umma, viongozi wa dini pamoja na wafanyabiashara mbalimbali.

Kufuatia uchunguzi uliofanywa na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali (CAG), Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilikuja na mapendekezo kadhaa ambayo yaliridhiwa na Bunge la Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania. Kati ya mapendekezo hayo ni kuwajibishwa kwa viongozi na watumishi wa umma waliohusishwa katika kashfa hii. Utekelezaji wa mapendekezo haya umekuwa wa kusuasua sana, ukiachilia mbali kujiuzulu na kutolewa madarakani kwa baadhi ya mawaziri.



**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

Pamoja na hayo, baadhi ya viongozi na watumishi wa umma waliitwa mbele ya Sekretarieti ya Utumishi wa Umma kwa ajili ya kuhojiwa juu ya uhusishwaji wao katika kashfa hii ya ESCROW. Baadhi ya viongozi na watumishi hawa walionyesha dharau dhidi ya Sekretarieti na umma wa watanzania kwa ujumla, kwa kutoa kauli za kejeli zilizohusiana na tuhuma zilizokuwa zinawakabili.

**Mapendekezo:**

Taarifa hii pia inaonyesha changamoto mbalimbali za haki za binadamu, ikiwa ni pamoja na hali ya rushwa, elimu, haki kupata maji safi na salama; Hivyo basi Kituo cha Sheria na Haki za Binadamu kinapendekeza yafuatayo;

(a) Vita dhidi ya ukatili na mauaji ya watu wenye ualbino igeukie pia kwa watuhumiwa wanunuzi wa viungo vya watu wenye ualbino badala ya kuangalia waganga wa kienyeji peke yake;

(b) Serikali ishirikiane na wadau mbalimbali kuhakikisha mkakati ambao utahakikisha ulinzi endelevu wa haki za watu wenye ualbino unakuwepo;

(c) Serikali inatakiwa iendelee kushirikiana na wadau mbalimbali kuhakikisha kunakuwa na mabadiliko na uboreshwaji wa sheria na miswada ya sheria inayogusa maslahi ya haki ya upatikanaji wa habari na uhuru wa kujieleza na wa habari; hususani Sheria ya Takwimu, Sheria ya Makosa ya Mtandaoni, Muswada wa Sheria ya Upatikanaji wa Habari na Muswada wa Sheria ya Vyombo vya Habari;

(d) Watuhumiwa wa makosa ya kujichukulia sheria mkononi na mauaji yanayotokana na imani za kishirikina washughulikiwe kama wahalifu wengine kwa mujibu wa sheria za nchi;

(e) Serikali ihakikishe kuwa mfumo wa upatikanaji wa Haki unaboreshwa ili kurudisha imani ya wananchi;

(f) Serikali ihakikishe kuwa vituo vya Polisi vinaboreshwa ili kuhakikisha ulinzi wa askari polisi wawapo kazini;

(g) Ngvu za ziada zichukuliwe kuhakikisha kuwa mianya ya rushwa inadhibitiwa katika sekta ya usafirishaji, ikiwa ni pamoja na kuhusisha umma katika kutoa taarifa ya uvunjifu wa sheria za barabarani na kutoa elimu kwa njia za kisasa;

(h) Serikali ihakikishe kuwa Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 inafanyiwa marekebisho ili kulinda maslahi na ustawi wa mtoto wa kike;

(i) Serikali ihakikishe inapata vyanzo mbadala vya uaptikanaji wa fedha kwa ajili ya huduma na vifaa vya afya katika hospitali za umma;

(j) Tume ya Taifa ya Uchaguzi iangalie uwezekano wa kurudia zoezi la uandikishwaji kwenye daftari la wapiga kura ili kutoa fursa kwa wale waliokosa fursa kujiandikisha kufanya hivyo, na hivyo kutekeleza haki yao ya kikatiba.



**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.

Mwisho kabisa nawatakia kila la heri katika harakati na kazi za kueneza na kukuza uelewa wa haki za bindamu, sheria na utawala bora. Vyombo vya habari vina nafasi kubwa sana kuhakikisha hili linafanikiwa ili tuweze kufikia jamii inayotaamali haki na usawa.

Nawashukuru sana kwa kunisikiliza.

Dr. Helen Kijo Bisimba
Mkurugenzi Mtendaji - LHRC



**Board of Directors:**
Prof. Geoffrey R.V. Mmari - *Chairperson*, Ms. Athanasia Soka (Adv) - *Vice Chairperson*, Dr. Helen Kijo-Bisimba - *Secretary*, Mr. Francis Stolla (Adv), Dr. Ringo W. Tenga (Adv), Ms. Maria Sarungi Tsehai, Ms. Diana Monica Kisaka, Prof. Chris Peter Maina, Ms. Emeline Mboya.